

## Maswali

1. Mbona Paulo alikaa Efeso kwa mda mrefu?
2. Sanamu ya Dina ilifaidisha watu wengine namna gani?
3. Mbona kununuliwa kwa mifano ya sanamu Kulididimia?
4. Demetrio alifanya nini kukataza watu wasimfwate Paulo?
5. Nini ilifanyika kwa mkusanyiko?
6. Paulo alitaka kufanya nini kuhusu mkusanyiko?
7. Nini ilifanyika kunyamazisha huo mkusanyiko?
8. Afisa aliambia watu wenye walikuwa wamesanyika nini?

## Majibu

1. Kwa sababu kulitakiwa kuwe na mahubiri mengi.
2. Watu walipata faida kwa kutengeneza mifano ya Dina kutoka kwa fedha na shaba na kuuza.
3. Kwa sababu Paulo aliwambia kwamba ni makosa kusujudia Dina au sanamu zingine zozote.
4. Alikusanya watu. Aliwahadharisha kwamba Paulo akiendelea hekalu itaharibiwa.
5. Kusanyiko lilikuwa na kelele nyingi hata marafiki wawili wa Paulo wakashikwa.
6. Paulo alitaka kwenda kuwanyamazisha lakini akazuiliwa na marafiki wake.
7. Watu walinyamaza wakati afisa mheshimiwa alitokea.
8. Aliwambia kwamba ilikuwa kinyume ya sheria kufanya ghasia kwa hivyo kama kulikuwa na malalamishi kuhusu Paulo, wapeleke mahakamani.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 1 Mwaka wa 2



# 50 Paulo ako Efeso

## Marejeo

Matendo ya Mitume 19:23-41

## Kiini cha somo


Neno la kweli la Mungu lazima lihubiriwe hata kama watu wanafuata miungu wengine.

## Maneno maalum

1. Sifa + Dina + sanamu
2. Sura (mfano) + ibada ya uongo + kazi haikuendelea.
3. Demetrio + kusanyiko + Paulo hatarini
4. Piga kelele + wawili washurutishwa + Paulo azuiliwa
5. Iskanda + piga kelele + mchafuko
6. Afisa + kimya + kinyume na sheria + mahakama
7. Ondoka

**50.1** Baada ya Paulo kutembelea wandugu wa Yerusalemu alirudi Efeso. Alikaa huko kwa miaka miwili. Kulikuwa na kazi nyingi ya kuhubiri. Efeso ulikuwa mji mzuri kwa eneo hiyo. Ulikuwa mji mkubwa na wa sifa. Walioishi kule waliabudu Dina mungu wa kike. Kulikuwa na hekalu hapo Efeso nzuri kubwa iliyotengewa Dina, ndani ya hekalu kulikuwa na sanamu kubwa ya Dina. Watu walisema kwamba hiyo sanamu ilikuwa imeanguka kutoka angani.

**50.2** Watu wengi walipata mapato yao ya kila siku kutumia sifa ya Dina. Kulikuwa na biashara kubwa kwa sanamu ndogo ya Dina iliyotengenezwa kutoka kwa fedha na shaba. Hizi sanamu ndogo zilikuwa mfano wa kubwa iliyoko hekaluni. Punde tu Paulo alifika Efeso. Alihubiri kwamba ni makosa kusujudia kitu chochote kilicho tengenezwa na mtu. Biashara ikaanza kudidimia. Watu wachache walinunua sanamu za Dina.



**50.3** Kulikuwa na mtu mmoja aliyetaka kumkataza Paulo. Jina lake ni Demetrio. Aliwaita fundi wote kwa kusanyiko moja. Watu walikuja wengi kwa huo mkutano. Aliwambia, “Kuna hatari kwamba huyo mtu atawageuza watu wa mkatae Dina. Hata hekalu itaharibiwa ikiwa watu watamsikiliza. Akawauliza, Mtapata namna gani mapato?”

**50.4** Watu walianza kuwa na wasi wasi wakapiga kelele na kusema, “Dina wa Waefeso ni mkuu.” Wengine wakaenda kumtafuta Paulo lakini hawakumpata.

Badala yake walichukuwa marafiki wake wawili Aristarko na Gayo na kuwapeleka kwa uwanja wa michezo. Walitaka kuwaumiza. Paulo aliposikia kilichokuwa kikitendeka alitaka kwenda kule na azungumze nao lakini marafiki wake walimkataza. Ilikuwa hatari sana.

**50.5** Wayahudi walisukuma mtu mmoja mbele ya mkusanyiko ili azungumze kwa niaba yao. Jina lake lilikuwa Askanda. Alikuwa mfua shaba. Umati ulipogundua kwamba yeye ni Myahudi hawakutaka kumsikiliza, wakapiga kelele tena na kusema, “Dina wa Efeso ni mkuu.” Kelele iliendelea kwa karibu masaa mawili. Kila mtu mjini alipiga kelele. Lakini watu wengine hawakujua ni kwa nini walipiga kelele kwa sababu marafiki wao walikuwa wakipiga kelele. Wengi hawakujua mchafuko ulikuwa juu ya nini.

**50.6** Hali ilikuwa mbaya. Mtu mmoja mwenye hatujui jina lake alikuwa jasiri sana. Alikuwa afisa wa mji. Ni kama watu walikuwa wanampenda kwa sababu alipofika tu wote walinyamaza kimya. Aliwambia, “Zote twajua vile Dina ni wa maana kwa Efeso. Lakini msifanye mambo yaliyokinyume na sheria. Malalamishi yenu juu ya hawa watu inatakiwa ipelekwe mahakamani iamuliwe na hakimu. Mko mnavunja sheria kwa kufanya ghasia.” Watu walifikiria juu ya maneno ya afisa wa mji na wakanyamaza kimya. Waliona kwamba wanafanya makosa kwa hivyo wakaenda nyumbani.

**50.7** Baadaye Paulo, aliamua kwamba hatahubiri Efeso tena wakati wa huu murupuko. Kwa hivyo aliaga marafiki wake na akaondoka.